

**KUMB: PPR/14 - 11/1**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA  
JUMATANO, TAREHE 5 Novemba 2014**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 5 Novemba 2014**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta aina zote, yaani, Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeshuka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 01 Oktoba 2014. Katika toleo hili, bei za rejareja kwa Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa viwango vifuatavyo; Petroli Sh 14/lita sawa na asilimia 0.66%, Dizeli Sh 37/lita sawa na asilimia 1.81% na Mafuta ya Taa Sh 22/lita sawa na asilimia 1.10% Kwa kulinganisha matoleo haya mawili, bei za jumla zimepungua kama ifuatavyo: Petroli, Sh 14.40/lita sawa na asilimia 0.69%, Dizeli, Sh 37.32/lita sawa na asilimia 1.90%, na Mafuta ya Taa, Sh 22.17/lita sawa na asilimia 1.16%. Kufuatia kushuka kwa bei za mafuta katika soko la Dunia, bei za mafuta katika soko la ndani zingepungua zaidi, isingekuwa ni kwa sababu ya kuendelea kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani.
- (b) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2008, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (c) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani ilimradi bei hizo ziko chini ya bei kikomo (price cap) kama ilivyokokotolewa na fomula iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 432 la tarehe 29 Novemba 2013.**
- (d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionyesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta kutoka kwenye vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja na adhabu itatolewa kwa kituo husika.**
- (e) Wanunuzi wanashauriwa kuhakikisha kuwa wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo; ama endapo utakuwa umeuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa.

## A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Sh/Lita)	Dizeli (Sh/lita)	Mafuta Ya Taa (Sh/Lita)
<b>Dar es Salaam</b>	2,178	2,027	1,993
<b>Arusha</b>	2,262	2,111	2,077
Arumeru (Usa West)	2,262	2,111	2,077
Karatu	2,280	2,129	2,096
Monduli	2,267	2,117	2,083
Ngorongoro (Loliondo)	2,318	2,168	2,134
<b>Kibaha</b>	2,182	2,032	1,998
Bagamoyo	2,189	2,038	2,004
Kisarawe	2,185	2,034	2,001
Mkuranga	2,187	2,037	2,003
Rufiji	2,205	2,055	2,021
<b>Dodoma</b>	2,236	2,086	2,052
Bahi	2,244	2,093	2,059
Chemba	2,263	2,112	2,078
Kondoa	2,269	2,119	2,085
Kongwa	2,234	2,083	2,049
Mpwapwa	2,238	2,087	2,053
<b>Iringa</b>	2,242	2,091	2,057
Kilolo	2,246	2,096	2,062
Mufindi (Mafinga)	2,252	2,101	2,067
<b>Njombe</b>	2,270	2,119	2,085
Ludewa	2,308	2,157	2,123
Makete	2,301	2,150	2,116
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,268	2,117	2,083
<b>Bukoba</b>	2,393	2,242	2,208
Biharamulo	2,367	2,217	2,183
Karagwe (Kayanga)	2,409	2,259	2,225
Kyerwa (Ruberwa)	2,415	2,264	2,230
Muleba	2,393	2,242	2,208
Ngara	2,358	2,208	2,174
Misenyi	2,401	2,251	2,217
<b>Geita</b>	2,343	2,192	2,158
Bukombe	2,332	2,181	2,147
Chato	2,364	2,213	2,179
Mbogwe	2,381	2,230	2,196

Nyang'hwale	2,358	2,207	2,173
<b>Kigoma</b>	2,409	2,258	2,224
Uvinza (Lugufu)	2,421	2,270	2,236
Buhigwe	2,398	2,247	2,213
Kakonko	2,366	2,215	2,181
Kasulu	2,395	2,244	2,210
Kibondo	2,373	2,222	2,189
<b>Moshi</b>	2,251	2,101	2,067
Hai (Bomang'ombe)	2,255	2,104	2,070
Mwanga	2,244	2,094	2,060
Rombo (Mkuu)	2,272	2,122	2,088
Same	2,238	2,087	2,053
Siha (Sanya Juu)	2,258	2,107	2,073
<b>Lindi</b>	2,236	2,086	2,052
Kilwa Masoko	2,212	2,061	2,027
Liwale	2,257	2,107	2,073
Nachingwea	2,266	2,115	2,081
Ruangwa	2,264	2,113	2,079
<b>Babati</b>	2,300	2,149	2,115
Hanang (Katesh)	2,310	2,160	2,126
Kiteto (Kibaya)	2,311	2,160	2,126
Mbulu	2,313	2,162	2,128
Simanjiro (Orkasumet)	2,332	2,181	2,147
<b>Musoma</b>	2,356	2,205	2,171
Rorya (Ingirijuu)	2,365	2,214	2,180
Bunda	2,347	2,197	2,163
Butiama	2,353	2,202	2,168
Serengeti (Mugumu)	2,401	2,251	2,217
Tarime	2,367	2,216	2,183
<b>Mbeya</b>	2,285	2,134	2,100
Chunya	2,294	2,144	2,110
Ileje	2,298	2,147	2,113
Kyela	2,300	2,150	2,116
Mbarali (Rujewa)	2,269	2,118	2,084
Mbozi (Vwawa)	2,294	2,143	2,109
Momba (Chitete)	2,303	2,152	2,118
Rungwe (Tukuyu)	2,294	2,143	2,109
<b>Morogoro</b>	2,203	2,052	2,018
Mikumi	2,218	2,068	2,034
Kilombero (Ifakara)	2,240	2,090	2,056
Ulanga (Mahenge)	2,251	2,101	2,067
Kilosa	2,221	2,071	2,037

Mvomero (Wami Sokoine)	2,213	2,063	2,029
Turian	2,228	2,077	2,043
<b>Mtwara</b>	2,250	2,100	2,066
Nanyumbu (Mangaka)	2,299	2,148	2,114
Masasi	2,276	2,125	2,091
Newala	2,282	2,132	2,098
Tandahimba	2,275	2,125	2,091
<b>Mwanza</b>	2,327	2,177	2,143
Kwimba	2,364	2,213	2,179
Magu	2,336	2,185	2,151
Misungwi	2,333	2,183	2,149
Sengerema	2,360	2,209	2,175
Ukerewe	2,387	2,236	2,202
<b>Sumbawanga</b>	2,350	2,200	2,166
Kalambo (Matai)	2,343	2,192	2,158
Nkasi (Namanyele)	2,364	2,213	2,179
<b>Katavi (Mpanda)</b>	2,385	2,235	2,201
Mlele (Inyonga)	2,364	2,213	2,179
<b>Songea</b>	2,301	2,150	2,116
Mbinga	2,334	2,184	2,150
Namtumbo	2,330	2,180	2,146
Nyasa (Mbamba Bay)	2,337	2,186	2,152
Tunduru	2,360	2,209	2,175
<b>Shinyanga</b>	2,306	2,156	2,122
Kahama	2,320	2,169	2,136
Kishapu	2,335	2,184	2,150
<b>Simiyu (Bariadi)</b>	2,348	2,197	2,163
Busega (Nyashimo)	2,341	2,190	2,156
Itilima (Lagangabilili)	2,351	2,200	2,166
Maswa	2,339	2,189	2,155
Meatu (Mwanhuzi)	2,346	2,196	2,162
<b>Singida</b>	2,268	2,118	2,084
Iramba	2,280	2,130	2,096
Manyoni	2,253	2,102	2,068
Ikungi	2,264	2,113	2,079
Mkalama (Nduguti)	2,293	2,142	2,108
<b>Tabora</b>	2,332	2,181	2,147
Igunga	2,286	2,135	2,101
Kaliua	2,350	2,199	2,165
Ulyankulu	2,344	2,193	2,159
Nzega	2,296	2,146	2,112
Sikonge	2,343	2,193	2,159

Urambo	2,345	2,194	2,160
<b>Tanga</b>	2,224	2,073	2,039
Handeni	2,203	2,053	2,019
Kilindi	2,238	2,087	2,053
Korogwe	2,217	2,066	2,032
Lushoto	2,226	2,076	2,042
Mkinga (Maramba)	2,238	2,088	2,054
Muheza	2,224	2,073	2,039
Pangani	2,230	2,080	2,046

**B: BEI ZA JUMLA**

<b>Bei za Jumla - DSM</b>	<b>Petroli (Sh/L)</b>	<b>Dizeli (Sh/L)</b>	<b>Mafuta ya Taa (Sh/L)</b>
<b>Bei Kikomo</b>	<b>2,075.73</b>	<b>1,925.25</b>	<b>1,891.38</b>

**Felix Ngamlagosi**  
**MKURUGENZI MKUU**  
**EWURA**